Wameangamia wenye kufanya uzito katika mambo

Kutoka kwa Abdallah Ibn Masoud amesema: Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Wameangamia wenye kufanya uzito katika mambo" Alisema hivyo mara tatu.

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu kufeli na kupata hasara kwa watiao ugumu -pasina uongofu wala kuwa na elimu- katika dini yao na dunia yao, na katika kauli zao na matendo yao, wenye kuvuka mipaka ya sheria aliyokuja nayo Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3420